13. Yesu anamwambia bibi yake wa Harusi – Wakati ni sasa ama si tena kamwe

Uaaminifu yako iko wapi bibi yangu wa harusi?

(English Title – Jesus says to His Bride… Now or Never)

Desemba 13th 2015 – Ujumbe kutoka Yesu kwa Dada Clare
Kutafsiriwa na Louis

Uko tayari kuiingia kwenye chumba chako cha kuomba na kunipa faraja, ama kwamba utakuwa kama watoto wangu wengine wanaoshugulika kwa maneno ya kununua, kuuza na kusherekea vitu vya dunia mwishowe. Utakuwa wapi kati yao? Utakuwa kwa jahazi langu ama kwenye cheo kubwa ukisifu vitu vya dunia?

Uaminifu wako uko wapi? Unaniamini mimi Yesu? Unajiamini mwenyewe? Au unaamini dunia na shetani? Ziko wapi zile vitu unazoamini sana? Ziko kwenye benki? Familia yako? Marafiki yako? Ziko kwangu Yesu wako? Uaminifu wako uko wapi bibi yangu wa harusi? Utakuwa wapi wakati ambapo utakapoambatana na mafuriko ya maji kuzidi kwa maisha yako?

Nakuita sahi uamue ni wapi utakaposimama. Nakuita bibi yangu wa harusi nikiwa na machozi, tafadhali, tafadhali, kuja na mimi kwenye jahazi langu la upendo, hapo utanipata nikiwa kwa mateso sana, na hapo pia ndipo nitakapokukinga. Naam, nateseka sana, na nitaendelea kuteseka hadi mabaya yatapotea kamili. Naam, nalia kwa uchungu kwa ajili ya bibi yangu wa harusi amabaye ameenda kwa duka za dunia kujiuza tena, akiniwacha kwa ajili ya vitu vya dunia zinazometameta.

Ujumbe huu ni rahisi sana, hakuna kitu kigumu kuihusu, nahitaji kuwa karibu na bibi yangu wa harusi, nahitaji faraja yake, nahitaji anishikilie kama mtoto mdogo na anipende, nahitaji kumwona akinipaka mafuta yake yenye utamu, nahitaji sauti yake safi inibembeleze nilale ili nipelekwe mbali kutoka maneno mengi ninayoyasikia na kuyaona kila siku.

Tafadhali bibi yangu wa harusi, wachana na vitu vya dunia kwa huu wakati wa utakatifu, kuja ndani yangu, kuja pahali pangu pa siri, njoo kwenye jahazi la upendo wangu, nisaidie kwa kuponya vidonda vyangu, nisaidie niweze kusahau wale watoto wangu wameniwacha kwa roho ngumu, wasionijali kamwe.

Huelewi vile napenda kukuona kwa muda mdogo tu bibi yangu wa harusi. Fikiria tu, uko penye pahali pa sherehe, ukiwa na watu wengi ambao wameungana kusherekea siku ya kuzaliwa ya Mfalme. Kila mtu anayeingia kwa mlango na kuenda penye mahali pa densi akiwaonyesha wengine uzuri wake, akitazamwa kwa upendo. Kila mtu amezubaishwa na fikira za vitu vya dunia, kama utajiri, kujulikana na watu wengi, vyeo vya juu, kutarajia kuwa bingwa, ujue zote ni mchezo ambao hauna mwisho.

Rudi tena kwa hiyo sherehe ya Mfalme, ghafla tu, watu wote waliozubaishwa kwa hiyo sherehe wanapinduka kutazama Mfalme akiingia kwa Mlango. Mflame anasoma fikira za watu wote kwenye hiyo sherehe. Watu wananungunika kwa ajili walikuwa wamezubaishwa kwa

sherehe na hawangependa kutozubaa kwa niaba ya Mfalme. Walakini, wanamwona Mflame kama amesimama, akiwa amevaa mavazi maarufu, kuwa yeye ni mkombozi wa dunia. Mfalme akiwaangalia wote, wakibaki bila kujua, anasoma fikira na hisia za watu wote waliokwenye hiyo sherehe.

Hapo kando kuna maua mzuri sana amejificha. Ni msichana ambaye hashuguliki na ubingwa, utajiri na vitu vya dunia. Ameshuguliika na uzuri na umaarufu wa Mflame pekee yake. Kushangazwa kwa uzuri wa roho yake, na pia kuwa huyu msichana ni tofauti na watu wengine, Mflame huyu anatembea kwa upande huyo msichana alipoketi na kumfikia. Anapomfikia anamwinua huyo msichana akiweka mkono wa huyo msichana kwa yake. Kisha Mfalme wa sherehe anatangaza ya kwamba, "Nimempata yule anayefaa kuwa Malaika wangu"

Watu wote kwa sherehe wamebaki kwa mshangao sana, midomo yao iko wazi, kimya inajaza shrehe mzima, malaika aliyechanguliwa ni mtu hajulikani kabisa! Angalia mavazi yake yasiyomazuri na familia yake si ya wafalme.

Nikiwaangalia, bibi wangu wa harusi, nalazimishwa kuona nini? Fikira na moyo zenu zitakuwaje? Utakosa kuwa mpole na mimi kwa ajili umezubaishwa na vitu vingi unavyotamani kuvinunua dukani kwa ajili wakati imedidimia…na huwezi ngoja kufika dukani? Ama utajazwa na hisia ya upendo kwa ajili Mflame wako yuko hapo na wewe? Huyu ndiye bibi ya harusi ninayemtafuta, kwa ajili ananipenda sana na hana wakati wa kupoteza ama nia yoyote ya kununua vitu dukani, walakini angependa kuwa na mimi tu. Angependa kunywa kutoka kikombe changu cha uchungu, kushinda kuungana na marafiki wake kukula chakula.

Niko hapa, nimefunikwa na huzuni kwa ajili ya vile dunia yako imeanguka…naam, nasema ni dunia yako kwa ajili haifanani na dunia yangu. Nahisi huzuni nyingi kwa ajili ya vitendo vitakavyokufanyikia ghafla tu, kwasababu hapatakuwa na njia pa kuiepuka. Nimemtafuta bibi yangu wa harusi kwa duka tofauti, vyumba ya kukula chakula, sherehe tofauti na nimempata akizubaishwa na wanaume wengine, akifanya vitendo vya ngono, akifurahia uchafu wa shetani aliyempatia, ili ajazwe na furaha. Nahisi uchovu sasa kwa kujaribu kumwita, kumtafuta, kumwomba, nimechoka sana. Kama unataka kurudi kwangu Yesu wako itabidi uharakishe sana, kwa ajili hakuna wakati uliobaki. Wakati ni sasa ama si tena kamwe bibi wangu wa harusi. Wakati ni sasa ama si tena kamwe. Wakati ni sasa ama si tena kamwe.